TOLEO LA MESSENGER LA TURATHI ZISIZOGUSIKA

UNESCO
United Nations Educational, Scientific and Cultural Organization

1945 – 60 – 2005

KITENGO CHA TURATHI ZISIZOGUSIKA
www.unesco.org/culture/ich

AGOSTI 2006 n° 3
ISSN 2071-7784






## Maafikiano ya 2003
**Kuidhinishwa na mataifa kufikia Agosti 9, 2006**

1 ALGERIA
2 MAURITIUS
3 UJAPANI
4 GABON
5 PANAMA
6 UCHINA
7 JAMHURI YA AFRIKA YA KATI
8 LATVIA
9 LITHUANIA
10 BELARUS
11 JAMHURI YA KOREA
12 USHELISHELI
13 JAMHURI YA KIARABU YA SYRIA
14 UMOJA WA MILKI ZA KIARABU
15 MALI
16 MONGOLIA
17 CROATIA
18 MISRI
19 OMANI
20 DOMINICA
21 HINDI
22 VIET NAM
23 PERU
24 PAKISTANI
25 BHUTAN
26 NIGERIA
27 ICELAND
28 MEXICO
29 SENEGAL
30 ROMANIA
31 ESTONIA
32 LUXEMBOURG
33 NICARAGUA
34 CYPRUS
35 UHABESHI
36 BOLIVIA
37 BRAZIL
38 BULGARIA
39 HUNGARY
40 JAMHURI YA KIISLAMU YA IRAN
41 JAMHURI YA MOLDOVA
42 YORDANI
43 SLOVAKIA
44 UBELGIJI
45 UTURUKI
46 BUKINI
47 ALBANIA
48 ZAMBIA
49 ARMENIA
50 ZIMBABWE
51 CAMBODIA
52 JAMHURI YA YUGOSLAV YA MACEDONIA YA AWALI
53 MOROCCO
54 UFARANSA
55 CÔTE D'IVOIRE
56 BURKINA FASO
57 TUNISIA
58 HONDURAS
59 SAO TOME NA PRINCIPE
60 ARGENTINA

# Kikao cha kwanza cha Mkutano Mkuu

## Halmashauri huru ya Maafikiano ya 2003 iliendesha mkutano wake katika Makao Makuu ya UNESCO kwenye kikao chake cha kwanza hapo Juni 2006


© Michel Ravassard/UNESCO

*Bw. Bedjaoui akitoa hutuba yake baada ya kuteuliwa kama mwenyekiti wa Mkutano Mkuu*

Mnamo tarehe 27, Juni 2006, Mkurugenzi Mkuu wa UNESCO Bw. Koïchiro Matsuura alifungua kikao cha kwanza cha Mkutano Mkuu wa Mataifa Wanachama wa Maafikiano hayo ya kulinda Turathi za Tamaduni Zisizogusika (ICH), uliofanyika katika Makao Makuu ya UNNESCO huko Paris. Katika hotuba yake, Bw. Matsuura aliwashukuru viongozi na wawakilishi wote kwa kuhudhuria kongamano lile na kuyakaribisha mataifa wanachama 44 katika jopo hilo, pamoja na wale waliohudhuria kama wachunguzi. Hawa ni Wawakilishi wa wanachama wa mataifa 73 na mashirika mengi yasiyo ya kiserikali yaliyohusishwa katika mradi huu wa kukusanya na kuvumbua turathi zisizogusika. Kadhalika, Mkurugenzi huyu aliwakumbusha waliohudhuria kwamba wingi wa tamaduni kwa wanadamu ni sawa na uanuwai wa kiasili. Bw. Matsuura alisisitiza umuhimu wa kulinda turathi za tamaduni zisizogusika na aliwapongeza wanachama wa mataifa wanachama kwa kujitolea kwao katika kufikia hatua hiyo ya kuidhinisha Maafikiano hayo.

Lilikuwa ni jambo la busara mno kwa Kongamano hilo kumkaribisha aliyekuwa Katibu Mkuu wa Umoja wa Mataifa Bw. Javier Perez de Cuellar. Bw. Perez Cuellar, ni shabiki mkubwa katika masuala ya tamaduni, na hali kadhalika alisimamia Ripoti ya Tume ya Ulimwengu ya Tamaduni na Maendeleo ya mwaka wa 1995, ambayo ilifungua mwamko mpya wa kuielewa mijadala kuhusu tamaduni, utofauti wa tamaduni na matokeo ya maendeleo. Shukrani zingine za dhati zilimwendea Mstahiki Bw. Mohammed Bedjaoui, Waziri wa Mambo ya Nje wa Algeria, kufuatia mchango wake mkubwa katika utayarishaji wa matini ya Kongamano hili na kama Rais wa jopo la Wataalamu wa Muungano kati ya Serikali za Mataifa Wanachama katika mwaka wa 2002 na 2003.

Wakati wa ufunguzi wa kongamano hili, hotuba zilitolewa na Mheshimiwa Bw. Kenji Kosaka, Waziri wa Elimu, Tamaduni, Michezo, Sayansi na Teknolojia wa Ujapani; aliyejitolea kudhamini kamati ya mkutano wa pili uliofuatia wa Maafikiano kati ya Serikali za Mataifa Wanachama; Balozi wa Mila za Mapokezi na Muziki wa UNESCO, Bi. Mehriban Aliyeva; Bw. Alpha Oumar Konare, Rais wa Tume ya Umoja wa Afrika, aliyewakilishwa na Bw. Kedebe Kassa; Mstahiki Bw. Musa Bin Jaafar Bin Hassan, Rais wa Kongamano Kuu; na Mstahiki Bw. Zhang Xinsheng, Rais wa Halmashauri Kuu ya UNESCO. Awamu ya kwanza ilimalizikia kwa kumchagua Bw. Bedjaoui kama Mwenyekiti wa Mkutano Mkuu, ambaye katika hotuba yake ya kuyakubali madaraka hayo, alielezea wawakilishi wa mataifa wanachama umuhimu uliopo katika kuzilinda turathi za tamaduni zisizogusika.

## Tahariri

Sehemu ya kwanza ya Mkutano huo Mkuu wa Mataifa Wanachama katika Kongamano la mwaka wa 2003, ilikuwa ndiyo hatua iliyoambatanisha maamuzi bora kuhusu turathi zisizogusika tokea kuanzishwa kwa Maafikiano hayo mnamo Aprili iliyopita. Kongamano hilo lililofanyika Paris kuanzia tarehe 27-29, mwezi Juni 2006, lilikuwa ndio chanzo cha maisha ya utendakazi wa makubaliano hayo ya 2003. Sehemu kubwa ya toleo hili la *Messenger* imeshughulikia umuhimu wa Kongamano hili.

Katika makala kuu ya toleo hili, tumeeleza kuhusu ufunguzi rasmi wa kikao hiki na Mkurugenzi Mkuu mbele ya wageni waheshimiwa na mamia ya wawakilishi wa Mataifa Wanachama, wanachama wengine wa mataifa wanachama na mashirika yasiyo ya kiserikali. Makala maalum katika ukurasa wa 2 na 3 yametoa muhtasari wa mijadala ya kimsingi na maamuzi yaliyoafikiwa.

Kongamano hilo lilichagua Afisi iliyo chini ya Mwenyekiti Bedjaoui. Katika taratibu za kanuni na sheria zilizopitishwa, Jopo hilo lilibuni mfumo mzuri wa kuwachagua wanachama wa Kamati maalum kati ya serikali za Mataifa Wanachama, ambayo inahusika katika utekelezaji wa makubaliano. Mfumo huu unahakikisha mgawo sawa wa maeneo ya kijiografia kwa wanachama wa Kamati. Ni katika siku ya mwisho ya Mkutano huo ambapo Kamati ya wanachama 18 ilichaguliwa.

Orodha ndefu ya ajenda inausubiri utendakazi wa Kamati ambayo itafanya kikao chake cha kwanza kufikia tarehe 18 na 19 Novemba 2006 huko Algiers. Kwa miaka ijayo, Kamati itahitajika kuunda, kati ya mambo mengine, sheria za matumizi ya Hazina, vigezo vya kuingiza majina kwenye orodha ya turathi, na pia mfumo kabambe wa kuyateua mashirika yatakayosaidia kwenye utoaji ushaurinasaha. Patahitajika msururu wa mikutano ya Kamati ya makubaliano hayo na Kongamano ili kuhakikisha kwamba Maafikiano hayo yanaanza kazi haraka iwezekanavyo. Tunatazamia kukabiliana vilivyo na changamoto za Mkataba huu.

*Rieks Smeets, Kitengo cha Turathi Zisizogusika*




© Hugues Sicard/UNESCO

# Matokeo ya Mkutano Mkuu - mwanzo mpya

## Masharti ya utaratibu wa utendakazi

Baada ya ufunguzi wa kufana na uchaguzi wa Mwenyekiti, Naibu Mwenyekiti na wahusika wengine, jukumu la kwanza la Jopo hilo ni kupitishwa kwa masharti ya utaratibu wa utendakazi, ambayo hutoa maamuzi ya masuala muhimu, la muhimu zaidi likiwa ni jinsi ambavyo wanachama wa Kamati maalum kati ya serikali za Mataifa Wanachama itakavyoteuliwa. Kongamano hilo lilikumbana na matatizo machache kuhusiana na kanuni zake nyingi, kama zilivyotayarishwa na Afisi yake Kuu. Hali hii iliwapata wengi wao kinyume cha matarajio yao kwani ilikuwa tofauti kabisa na desturi za utendakazi walizozizowea za UNESCO, na hususan masharti ya utaratibu wa utendakazi wa Mkutano Mkuu kuhusu Maafikiano ya Turathi za Ulimwengu.

| MAKUNDI YA UCHAGUZI YA UNESCO | |
|---|---|
| Kikundi cha I | Uropa Magharibi |
| Kikundi cha II | Uropa Mashariki |
| Kikundi cha III | Latini Amerika na Caribbean |
| Kikundi cha IV | Asia na Pacific |
| Kikundi cha V(a) | Mataifa ya Afrika |
| Kikundi cha V(b) | Mataifa ya Uarabuni |

Sehemu muhimu ya sheria zilizopendekezwa ilikuwa ni pendekezo la kupanga uchaguzi wa Kamati kulingana na Kifungu cha 6.1 cha Maafikiano hayo kinachotoa maelezo kuhusu utengaji wa viti vya wanakamati kulingana na uwakilishi wa maeneo ya kijiografia. Pendekezo hili lilijadiliwa kwa kirefu. Kongamano hilo lilikubaliana kwa pamoja kwamba mfumo wa UNESCO wa kupiga kura kwa vikundi utatumiwa kama msingi bora wa kugawanya idadi maalum ya viti kwa makundi ya upigaji kura (*tazama sharti la 13.1 kwenye jedwali lililoambatishwa hapo chini*).

| SHARTI 13: UGAWANYAJI WA MAENEO YA KIJIOGRAFIA | |
|---|---|
| 13.1 | *Uchaguzi wa wanachama wa Kamati utafanywa kulingana na mfumo wa uchaguzi wa makundi ya UNESCO, kama ilivyopitishwa na Kongamano Kuu la UNESCO kwenye kikao chake cha hivi majuz. Kwa kufanya hivyo, ni ili ieleweke kwamba "Kikundi cha V" kitahusisha vikundi viwili tofauti vya wanachama kutoka Afrika na Mataifa ya Kiarabu.* |
| 13.2 | *(i) Viti 18 vya wanakamati vitagawanywa katika makundi ya wapiga kura kwa viwango vya idadi ya Mataifa Wanachama kutoka kwa kila kikundi, hivyo basi, baada ya mgawo huo, itakuwa angalau viti viwili vimetengewa kila kikundi.*<br><br>*(ii) Baada ya idadi ya Mataifa Wanachama kufika 24, viti hivyo vitagawanywa katika makundi ya upigaji kura kwa viwango vya idadi ya Mataifa Wanachama kutoka kwa kila kikundi, hivyo basi, baada ya mgawo huo, itakuwa angalau viti vitatu vimetengewa kila kikundi.* |

## Kamati ya muungano kati ya serikali za mataifa wanachama

**Uhusika**

Maafikiano haya yanapendekeza kuwepo kwa Kamati yenye wawakilishi 18 kutoka kwa Mataifa Wanachama na idadi hiyo kuongezwa hadi 24 wakati Mataifa Wanachama wa makubaliano haya itafikia 50. Itakumbukwa kwamba Maafikiano haya yataanza utendakazi wake kwa taifa husika miezi mitatu tu, na baada ya hapo taifa hilo litahitajika kufikisha ukubalifu wake kwa UNESCO.

Kwa sababu taifa la Zimbabwe lilikuwa ni taifa la tano kuandikishwa katika UNESCO, maamuzi yake ya kuwa mwanachama mnamo tarehe 30, Mei 2006, ni kwamba Maafikiano haya yatakuwa na wanachama 50 kufikia mwezi Agosti 2006.

Mataifa mengi Wanachama yaliutafsiri *uwakilishi huo wa mgawo wa kijiografia* kwenye Kamati kumaanisha kwamba viti hivyo vinafaa kugawanywa *sawa kwa sawa* katika makundi yote. Kwa mfano, viti vitatu kwa kikundi cha wanakamati 18, na viti vinne kwa Kamati ya wanachama 24. Mataifa mengine yaliunga mkono mapendekezo ya jopo hilo kutenga viti kulingana na idadi ya Mataifa Wanachama kwa kila kikundi cha upigaji kura.

Chaguo hili hatimaye lilipitishwa bila purukushani. Hata hivyo, katika kila uchaguzi, idadi ya viti kwa kila kikundi itabidi ihesabiwe upya, kwa kuzingatia idadi kamili ya mataifa wanachama katika Mkutano Mkuu na usambazaji wake kwenye makundi ya upigaji kura.

Kisha Kongamano hilo lilijadili iwapo, baada ya kuhesabu upya viwango vya mgawo huo, idadi ya chini ya viti inafaa kutengewa kila kundi. Afisi Kuu ya jopo ilikuwa imependekeza kutenga viti viwili kwa kila kikundi cha uchaguzi kwa kamati zote mbili, ile ya wanachama 18 na ile ya 24. Baada ya mdahalo mkali, jopo hilo liliamua kutoa nafasi ya viti viwili kwa kikundi cha Kamati ya wanachama 18 na viti vitatu kwa wanachama 24.

Wawakilishi wengine walipendekeza kwamba idadi kamili ya viti inafaa kutengwa. Pendekezo la mjadala mmoja uliojadiliwa kirefu ni kwamba ile Kamati ya wanachama 24 itengewe viti vitano. Mjadala huo utaendelea katika kikao kijacho. Idadi kamili itakapofahamika, sura moja itaongezwa katika sheria ya 13.2 ya Masharti ya Utaratibu wa Utendazi ya Kongamano Kuu (tazama jedwali lililoko sehemu ya kushoto kwenye ukurasa huu). Baada ya hatua hizi kuchukuliwa, jopo kuu la Kongamano liliweza kupitisha na kuidhinisha masharti hayo ya utaratibu wa utendakazi.

Kushoto, *Mkutano Mkuu wa wajumbe wote*
Chini *(safu ya mbele), Bw. Bedjaoui, Bi. Aliyeva, Bw. Matsuura, Bw. Bin Hassan*
Kulia, *mjumbe wa Bulgaria akipiga kura yake kwa uchaguzi wa Kamati maalum kati ya serikali ya Mataifa Wanachama.*



© Michel Ravassard/UNESCO



© Hugues Sicard/UNESCO

**Kuzaliwa kwa Kamati**

Siku ya kikao cha mwisho cha mkutano, wajumbe na wachunguzi walikuwa tayari kuendelea na suala muhimu katika ajenda: uchaguzi wa wanachama 18 wa Kamati ya kwanza, ambayo itahusika na utekelezaji wa Maafikiano. Uchaguzi ulianza Alhamisi Juni 29 mwendo wa saa sita mchana na kuchukua muda usiozidi saa mbili.

Washiriki wa mataifa walikuwa wamepewa tarehe ya mwisho kuwa (Juni 20) ya kutangaza ugombeaji wao kwa Kamati; kufikia mwisho wa siku hiyo, ofisi kuu ya utawala ilikuwa imepokea washiriki 30 wa uteuzi. Muda mfupi kabla ya uchaguzi, ujumbe wa kutoka Luxembourg, Mali, Mauritius, Misri, Jordan na Siria, kufuatia mashauriano katika makundi yao , ulijulisha jopo la mkutano kuhusu kujiondoa kwao katika kinyang'anyiro hicho cha ugombeaji. Kwa sababu hiyo, kulikuwa na wagombeaji wengi kulingana na nafasi zilizokuwa katika kundi la 1 na kundi V(b). Mkutano huo Mkuu kisha uliendelea na uchaguzi wa makundi manne yaliyobakia.

Wawakilishi 44 wa Mataifa Wanachama (kati ya 45) yaliyokuwa katika mkutano huo walipewa bahasha zilizokuwa na makaratasi manne ya kura, bahasha moja kwa kila kundi kwenye makundi hayo manne. Makaratasi yote 176 ya kupigia kura yalirudishwa; yote yalikuwa halali na hakuna wawakilishi waliokosa kupiga kura.

| MATAIFA YA KWANZA 18 YA WANACHAMA WA KAMATI MAALUM KATI YA SERIKALI ZA MATAIFA WANACHAMA | |
|---|---|
| Kundi I | Ubelgiji, Uturuki |
| Kundi II | Bulgaria, Estonia, Hungary, Romania |
| Kundi III | Brazil, Mexico, Peru |
| Kundi IV | Uchina, Hindi, Ujapani, Viet Nam |
| Kundi V(a) | Gabon, Nigeria, Senegal |
| Kundi V(b) | Algeria, Umoja wa Milki za Kiarabu |

**Masharti ya Ofisi ya Utawala**

Kimsingi, kipindi cha wanachama wa Kamati ni miaka minne; hata hivyo Maafikiano haya yanaeleza kwamba kwa misingi ya kuendeleza shughuli vyema, nusu ya uanachama itateuliwa upya baada ya kila miaka miwili. Kwa sababu hiyo, baada ya uchaguzi wa kwanza, mambo mengi yanastahili kupigiwa darubini ili kuchagua wanachama ambao watahudumu kwa miaka miwili peke yake kwenye Kamati hiyo. Jopo la Mkutano Mkuu liliamua kwamba utaratibu huu wa mara moja utafanyika katika kikao chake cha mkutano wa kwanza usio wa kawaida mnamo (Novemba 9).

## Hazina ya Kulinda Turathi za Tamaduni Zisizogusika

Jopo la Mkutano Mkuu lilijadili suala la mchango wa Mataifa Wanachama kwa Hazina ili Kulinda Turathi za Tamaduni Zisizogusika. Kwa pamoja, jopo la Mkutano Mkuu lilikubali kuweka mchango kwa asilimia 1 ya mchango wa Mataifa Wanachama kwa bajeti ya kawaida ya UNESCO.

Kwa kufanya hivyo, Mkutano Mkuu ulitekeleza Kifungu cha 26.1 cha Maafikiano, huku ukitumia asilimia ya juu zaidi inayoruhusiwa. Kulingana na hali ya sasa ya uidhinishaji, mchango wa mwaka kwa Hazina utajumlisha dola 1,100,000 za Marekani.

Jopo hilo la Mkutano Mkuu pia lilikubali kulinganisha mapato ya mchango na mpango wa miaka miwili wa UNESCO. Liliamua kwamba jukumu la kuchangia katika Hazina ya Mataifa Wanachama, litaanza rasmi pindi tu Maafikiano haya yatakapoanza utekelezaji wake.

Mwongozo wa matumizi ya Hazina utatayarishwa na Kamati maalum kati ya Serikali za Mataifa Wanachama, lakini Maafikiano hayo yanaonyesha sehemu muhimu za kupewa kipaumbele ambazo zitafadhiliwa kutoka kwa Hazina, na ambazo ni pamoja na usaidizi wa kimataifa wa kulinda turathi ambao umeandikwa katika Orodha ya Turathi za Tamaduni Zisizogusika Zinazohitaji Ulinzi wa Haraka, utayarishwaji wa orodha na Mataifa Wanachama, na usaidizi katika mipango ya ulinzi, miradi na shughuli nyinginezo.

## Kikao Kisicho cha Kawaida cha Mkutano Mkuu: Paris, Novemba 9, 2006

Ili kuichagua Kamati ya Mataifa sita Wanachama, Mkutano Mkuu uliamua kufanya kikao kifupi kisicho cha kawaida katika Makao Makuu ya UNESCO. Masuala yaliyokuwa katika ajenda yalihusisha: majadiliano ya mwisho kuhusu idadi ya juu zaidi ya viti ambavyo vitatengewa kila kundi la uchaguzi katika uchaguzi wa Kamati maalum kati ya Serikali za Mataifa Wanachama; uchaguzi wa wanakamati sita zaidi; na uchaguzi wa nusu ya wanachama 24 ambao watakuwa katika Kamati kwa kipindi cha miaka miwili.

MCHAPISHAJI Idara ya Turathi za Tamaduni Zisizogusika (ITH)
Sekta ya Tamaduni, UNESCO
1 Rue Miollis
75732 Paris Cedex 15, Ufaransa
Barua pepe: ich@unesco.org
Kipepesi: +33 (0) 145685752

MHARIRI MKUU Rieks Smeets

JOPO LA UHARIRI Fernando Brugman, Joan Fleming, Richard Lo Giudice, Reiko Yoshida

MWANA-RUWAZA Jean-Luc Thierry

***Tolea la Turathi za Tamaduni Zisizogusika*** linapatikana katika nakala zilizochapishwa na zile za kielektroniki katika lugha za Kiingereza, Kifaransa na Kihispania.

Matini yote inaweza kuopolewa katika wavuti (www.unesco.org/culture/ich) na kuchapishwa bila malipo bora tu wahusika wa habari hiyo waweze kutambuliwa.



© Conselho das Aldeias Wajãpi-Apina

# turathi zisizogusika


## KALENDA

**NOVEMBA 9** Kikao cha kwanza kisicho cha kawaida cha Mkutano Mkuu wa Mataifa Wanachama katika Kongamano la 2003, la UNESCO, Paris.

**NOVEMBER 18-19** Kikao cha kwanza cha Kamati maalum kati ya Serikali za Mataifa Wanachama ya Kulinda Turathi za Tamaduni Zisizogusika. Algiers, Algeria.

Kwa habari zaidi, wasiliana nasi kupitia: ich@unesco.org

## IMECHAPISHWA HIVI MAJUZI




Mnamo mwezi Juni, Kitengo cha Turathi Zisizogusika kilichapisha kijitabu cha kurasa 107 ambazo ziligusia kwa kina Vito vya Masimulizi na Turathi Zisizogusika za Kibinadamu zilizopatikana mnamo mwaka wa 2001, 2003 na 2005. Kuanzia matambiko, maonyesho na desturi za kuongea, hadi kwa desturi za kijamii, usanii, habari za kitamaduni, na nafasi za kitamaduni, vito hivyo vinatoka katika kila pembe ya ulimwengu na kuonyesha jinsi Turathi za Tamaduni Zisizogusika zilivyopanuka kote ulimwenguni. Kijitabu kimeelezwa kwa picha zaidi ya 100 zenye rangi na makala zinazoeleza juu ya kila kito cha thamani.

Chapisho hilo liliwezekana na hata tunawapa shukrani Serikali ya Ujapani kwa usaidizi wa kifedha katika mpango wa mradi uliopatiwa jina, "Shughuli za Upokeaji wa Matayarisho na Usimamizi wa Tatu wa Vito vya Masimulizi na Turathi Zisizogusika za Kibinadamu" yaani *Preparatory and Follow –up activities for the Third Proclamation of Masterpieces of the Oral and Intangible Heritage of Humanity*. Chapa za Kifaransa na Kiingereza tayari zinapatikana na tafsiri za Kihispania na Kijapani zinatayarishwa. Chapa ya Kiarabu, iliyofadhiliwa na Halmashauri ya Tamaduni na Turathi ya Abu Dhabi (Muungano wa Imarati), pia imepangwa. Chapa ya elektroniki zinaweza kupakuliwa kutoka katika mtandao mpya wa

Turathi za Tamaduni Zisizogusika (ICH) kupitia (www.unesco.org/culture/ich_convention). Idadi ndogo ya vijitabu inaweza kupatikana kupitia kwa maombi.

(*Vito vya Masimulizi na Turathi Zisizogusika za Kibinadamu. Vilitangazwa mwaka wa 2001, 2003 na 2005.*) Kimechapishwa na Kitengo cha Turathi Zisizogusika, Sekta ya Utamaduni ya UNESCO, Paris, Juni 2006.

## HABARI ZA TURATHI-HAI

**Kwa kutekeleza majukumu yake kama chombo cha kimataifa cha ubadilishanaji wa turathi za kitamaduni zisizogusika, UNESCO inaunda wavuti mpya na kituo rasmi cha kuakibisha au hifadhi nyaraka.**

### MTANDAO WATURATHI ZA TAMADUNI ZISIZOGUSIKA
**www.unesco.org/culture/ich_convention**

Katika kipindi cha kwanza cha Mkutano Mkuu mnamo Juni 2006, Kitengo cha Turathi Zisizogusika kilizindua mtandao mpya unaoeleza shughuli za UNESCO katika masuala ya Turathi za Tamaduni Zisizogusika (ICH).

**Nini shabaha ya wavuti huo?**
Wavuti huo mpya unalenga kuwa kituo maalum cha kimtandao kitakachosaidia usakuraji kwa lengo la kutangaza na kulinda turathi zisizogusika kote ulimwenguni kulingana na mpango na malengo ya Maafikiano ya 2003.

**Wateja wetu ni kina nani?**
Mtandao huo unalenga kuwa chombo muhimu kwa umma na watu wote wanaotaka kulinda na kusambaza habari kuhusu Turathi za Tamaduni Zisizogusika (ICH): maafisa wa serikali, mashirika yasiyo ya serikali, walimu, wanafunzi na wanachama wa jamii zinazohusika, pamoja na vyombo vya habari.

**Ni nini kinachoweza kupatikana kwenye wavuti huo?**
Habari kuhusu:
- Historia na maendeleo zaidi ya Maafikiano, Maswali Yanayoulizwa Mara kwa Mara (FAQ);
- Utendaji kazi wa Maafikiano: Mataifa Wanachama, mashirika ya serikali na mikutano yao, ufadhili wa kimataifa n.k;
- Ulinzi wa mipango, desturi njema, na miradi;
- Sheria zinazohusiana na Turathi za Tamaduni Zisizogusika (ICH), Sera, taasisi maalum, miradi na shughuli katika nchi mbali mbali. Maelezo ya nchi huwa yanaboreshwa kila wakati.

**Naweza vipi kuchangia katika wavuti huo?**
Mataifa Wanachama, mashirika yasiyo ya serikali na wadau wengine wanakaribishwa kututumia habari muhimu kuhusu taasisi, hatua na utendakazi bora unaohusiana na kufahamika, utangazaji na ulinzi wa turathi za tamaduni zisizogusika (ICH) katika nchi zao. Wafanyakazi wetu watakuwa wanaboresha wavuti mara kwa mara. Tunatambua ya kwamba ripoti ya 2003 inatafsiriwa kwa lugha nyingi na tutafurahia kuzichapisha katika wavuti wetu. Tafadhali wasiliana nasi kupitia: ich@unesco.org

### KITUO CHA KUHIFADHI NYARAKA ZA TURATHI ZA TAMADUBI ZISIZOGUSIKA KITAFUNGULIWA KATIKA MSIMU WA KUPUKUTIKA KWA MAJANI "AUTUMN" MWAKA WA 2006

Mbali na kuzindua wavuti mpya, Kitengo cha Turathi Zisizogusika kitafungua kituo cha kuhifadhi na kuakibisha nyaraka ambacho kitazingatia masuala ya Turathi za Tamaduni Zisizogusika (ICH) msimu wa majani kupukutika. Katika kituo hicho kipya kilichoko kwenye Makao Makuu ya UNESCO (Jengo la Bonvin, orofa ya 9), wageni wanaweza kukagua:
- Nyaraka muhimu kuhusu mikutano ya wataalam, mikutano ya muungano kati ya serikali za Mataifa Wanachama na mipango ya UNESCO katika masuala ya (ICH), kama mpango wa Vito-Hai vya Thamani vya Wanadamu;
- Habari kuhusu shughuli zinazohusiana na 'ICH' na mipango kabambe kote ulimwenguni;
- Makala, kabrasha, vitabu, video, SIDII-ROMU, DIVIDII na vitu vingine vilivyokusanywa katika miaka ya hivi karibuni kutoka sehemu tofauti na kupangwa kulingana na nchi.

Kitengo cha Turathi Zisizogusika kinakaribisha michango ya aina yoyote ya mambo yanayohusiana na Turathi za Tamaduni Zisizogusika 'ICH'. Kituo cha Nyaraka za Turathi za Tamaduni Zisizogusika kitafunguliwa kwa umma kuanzia 3.30 asubuhi hadi saa 7 mchana kwa siku za kazi za UNESCO. Tunatazamia kuwa utatutembelea. Kwa habari zaidi, wasiliana nasi kupitia: ich@unesco.org